

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**  
**MKOA WA MWANZA**

Shule ya Sekondari Shishani,  
S.L.P 306,  
Magu.  
18.12.2020

Kumb. Na SHSS/JI/2020

Ndugu \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SHISHANI (KUTWA)**  
**KIDATO CHA KWANZA-2021**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **Shishani** mwaka 2021. Shule ya sekondari Shishani iko katika kijiji cha Shishani, kata ya Shishani; umbali wa **km 40** Mashariki mwa mji wa Magu, Shule iko kandokando ya barabara iendayo Magu na Mahaha.

**Shule ya sekondari Shishani** ni ya kutwa kwa wanafunzi wa kidato cha **Kwanza** hadi cha **Nne**. Pia shule ni ya mchanganyiko kwa wanafunzi wote yaani wavulana na wasichana wanasoma kwa pamoja.

**Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni siku ya Jumatatu saa 1.30 Asubuhi na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021** (siku saba baada ya kuanza masomo). Baada ya muda huo kuisha utakuwa umepoteza nafasi hii adimu.

Masomo yanayofundishwa katika shule hii ni kumi na mbili (12) ambayo ni Kiingereza, Civics, Historia, Kiswahili, Geography, Hisabati, Fizikia, Kemia, Bailojia, Physical education, Commerce na Book keeping. **Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili.**

Kila mwanafunzi wa kidato cha kwanza atasoma wiki Sita(06) za kwanza za kozi maalumu ya somo la kiingereza (English Course) ili kumpatia msingi imara wa lugha ya Kiingereza.

**2.SARE ZA SHULE**

**(a) Wavulana waje na**

- (i). Suruali mbili zenye rangi ya dark bluu, zenye marinda mawili (02) kila upande zenye upana wan chi 18-22 chini ya miguu. Pia mifuko miwili ya kurosi na mfuko mmoja wa nyuma upande wa kulia.
- (ii). Mashati mawili(02) meupe yenye mikono mifupi.
- (iii). Jozi mbili (02) ya viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu, vyenye sole fupi na vinavyofungwa kwa gidamu (kamba) nyeusi. **Visiwe buti.**
- (iv). Jozi mbili za soksi nyeusi fupi zenye urefu kama penseli.
- (v). Mkanda mweusi wa ngozi usio na mapambo yoyote
- (vi). Sweta rangi ya bluu.

### **(b) Wasichana waje na**

(i). Sketi mbili (02) zenye rangi ya dark bluu, zisiwe na michirizi upande wa mbele, mkanda wa sketi uwe nchi mbili, marinda ya sketi yawe inchi mbilimbili na iwe na urefu wa kufika kwenye kifundo cha mguu(ankle).

(ii). Mashati mawili (02) meupe yenye mikono mifupi,

NB. Kwa waislam, sare ni sketi ndefu yenye rangi ya dark bluu, mashono, mtindo na idadi ni kama ilivyoelekezwa hapo juu (i).

Shati ni half kanzu (nusu kanzu) mikono mifupi kitambaa aina ya halua ama tomato, pamoja na juba jeupe linalofunika mikono, kitambaa aina ya halua ama tomato. Idadi kama ilivyoelekezwa hapo juu (ii)

(iii). Jozi mbili(02) ya viatu vya ngozi vyeusi vinavyofunika miguu, vyenye sole fupi na vinavyofungwa kwa gidamu (kamba) nyeusi.

(iv). Jozi mbili (02) za soksi nyeupe fupi zenye urefu kama penseli.

(v). Sweta rangi ya bluu

(vi). Blauzi mbili (02) nyeupe.

### **(c) Sare za michezo**

Kila mwanafunzi aje na T-shirt moja rangi ya damu ya mzee yenye kola, full tracksuit ya bluu bahari na viatu vya raba.

### **3. MAHITAJI YA DARASANI**

(i) Daftari kubwa za kawaida au kaunta zisizopungua kumi na mbili

(ii) Mkebe wa hisabati

(iii) Kalamu za wino za rangi ya bluu/nyeusi za kutosha

(iv) Kamusi ya lugha ya Kiswahili

(v) Kamusi ya lugha ya kiingereza

(vi) Four figure (Mathematical table).

(vii) Begi la kubebea madaftari (**mifuko mingine hairuhusiwi**)

**NB: Mzazi/mlezi anatakiwa alete chakula cha mwanafunzi pia nauli ya kuja na kutoka shuleni pamoja na matibabu ni juu ya Mzazi/Mlezi.**

### **4. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha na sheria Na. 10 ya mwaka 1995.

Aidha inazingatia miongozo yote ya inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI; yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalizi ya jioni (kujisomea binafsi) ni lazima
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa shuleni.
- e) Kufahamu mipaka ya shule, kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi binafsi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule ni lazima.
- g) Kuvaa sare ya shule inayotakiwa na inavyotakiwa kuvaliwa muda wote.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kutunza mali za umma

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.**

1)Uasherati (2) Utoro (3) Kudharau Bendera ya Taifa, Wimbo au fedha za Taifa  
(4) Kupiga/Kupigana (5)Kuharibu kwa makusudi mali ya umma (6)Ulevi wa aina yoyote (7)  
Kutumia au kuwa na madawa ya kulevya (8)Kujihusisha na mambo ya kishirikina (9) Matusi kwa  
walezi hapa shuleni, viranja, wanafunzi wenzake au kwa yeyote yule (10)Wizi (11)Kupata mimba ama  
kusababisha mimba (12)Kutoa mimba (13) Kulala nje ya shule (14)Makosa yenye kujirudiarudia (15)  
Kukataa kufanya adhabu (16)Kuongoza migomo au fujo yeyote shuleni (17) Kuvuruga Amani ya  
jamii ya shule (18) Ubakaji (19) Makosa ya jinai.

**5. MAMBO MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

Mwanafunzi anapokuja shuleni kuripoti aje na

- (i). Fomu ya Hospitali iliyojazwa kikamilifu na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali
- (ii). Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
- (iii). Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengineyo.

**MUHIMU: FOMU HIZI ZIMEAMBATISHWA PAMOJA NA BARUA HII NA ZIKAMILISHWE KAMA ILIVYOELEKEZWA.**

**KILA MZAZI AFIKE KURIPOTI AKIWA NA MWANAYE LA SIVYO HATAPOKELEWA SHULENI.**

**Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu KAULI MBIU YA SHULE YETU YA SHISHANI NI “JUHUDI NA MAARIFA”**

**Nakutakia utekelezaji mwema,**

**KARIBU SANA SHULENI SHISHANI SEKONDARI**

**EDWARD M. NDAMA  
MKUU WA SHULE**

**MKUU WA SHULE  
SHULE YA SEKONDARI SHISHANI  
MAGU**

# HALMASHAURI YA WILAYA MAGU

## SHULE YA SEKONDARI SHISHANI

S.L.P 306, MAGU

### KIAMBATANISHO A

### HISTORIA NA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

#### 1. MAELEZO BINAFSI

Jina la mwanafunzi.....

Majina ya wazazi

(i)Baba.....(hai/amefariki)

(ii)Mama..... (hai/amefariki)

Kabila la mwanafunzi..... Dhehebu la dini yake.....

Tarehe ya kuzaliwa.....wilaya/nchi alikozaliwa.....uraia wa nchi ya.....

Uhusiano na mlezi.....

Kazi ya Mzazi/Mlezi.....

Sehemu/ofisi anayofanyia kazi mzazi/Mlezi.....

Idadi ya ndugu katika familia (i)wa kike.....(ii)Wa kiume.....(iii)wategemezi.....

Ni wangapi kuzaliwa katika familia..... Afya yake kwa ujumla.....

Matatizo maalumu aliyonayo mwanafunzi kitabia na kiafya .....

.....

Uwezo/kipaji maalumu alivyonavyo mwanafunzi .....

#### 2. SHULE ALIZOSOMA

SHULE	WILAYA/NCHI	MADARASA	MIAKA
1.			
2.			
3.			
4.			
5.			
6.			

#### 3. MAELEZO YA NYONGEZA KAMA YAPO.....

.....  
.....

Bandika picha

Moja ya

Mwanafunzi

Awe na shati  
jeupe la shule

**MAGU DISTRICT COUNCIL  
SHISHANI SECONDARY SCHOOL  
P.O.BOX 306 MAGU**

**KIAMBATANISHO B**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**(To be completed by Medical officer in respect to all form of entrants)**

Student's full name.....

Age (Years).....

Blood count (red and white).....

Stool examination.....

Urine analysis.....

Syphilis and other venereal diseases test.....

T.B Test.....

Eye Test.....

Ears .....

Chest Examination.....

Spleen .....

Abdomen .....

Test for pregnancy.....

ANY ADDITIONAL INFORMATION e.g Physical defect, chronic or Family diseases etc

.....

.....

I certify that the person named above is fit/unfit to pursue further studies in secondary education

Station .....

Signature .....

Designation .....

Date .....

❖ Delete where necessary:

**HALMASHAURI YA WILAYA MAGU**  
**SHULE YA SEKONDARI SHISHANI**  
**S.L.P 306 MAGU**

**KIAMBATANISHO C**

**AHADI YA KUTII SHERIA AMRI NA MAMLAKA YA SHULE**

Mimi(Mwanafunzi).....nimesoma kwa makini sheria zote za shule. Nimezielewa barabara na nakubali kwa hiari yangu kuzitii na kuziheshimu. Nitafanya kazi na kusoma kwa bidii ili kujijengea msingi bora wa maisha yangu ya baadaye ili kujiletea heshima na sifa yangu binafsi kwa ujumla. Wakati wote nikiwa shuleni sitajihusisha na utoro, uchelewaji na mambo mengine yaliyo kinyume na taratibu, sheria na kanuni za shule. Daima nitakuwa mtiifu kwa wanafunzi wenzangu, viongozi wa serikali ya wanafunzi, mamlaka ya shule na jamii nzima kwa ujumla.

Ndimi mwanafunzi (jina).....

Saini.....Tarehe.....

~~~~~

**KIAMBATANISHO D.**

Mimi.....Mzazi/Mlezi nimesoma sheria na taratibu za Shule. Nimezielewa nami nakubali mwanangu/kijana wangu ajiunge/asijiunge na masomo katika shule hii, na kuwa nitakubaliana na adhabu yoyote itakayotolewa hasa pale mwanangu atakapohibitika kuwa amegoma, amechochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

Ndimi mzazi/Mlezi (jina).....



Saini.....Namba za simu za wazazi/walezi  
.....Tarehe  
.....

2.0 Mambo ya muhimu ya kuzingatia:-

2:1 Sare ya shule,

a) Sare ya shule hii ni kama ifuatavyo:- Mchoro wa mashono

### SURUALI ISHONWE HIVI




Upana usizidi inchi 18.  
na usipungue inchi 16.

### Vipimo (suruali)

- Upana usizidi nchi - 18
- Luksi -ziwe sita tu
- Mfuko wa nyuma mmoja tu.

### SKETI ISHONWE HIVI



Belt nchi 2.

Malinda nchi 2